
World Vision



# USAWA WA **KIJINSIA** NA UHUSISHAJI **WA KIJAMII**

# Mkabala na Nadharia ya Mabadiliko

2023 | 2nd EDITION



## YALIYOMO


**Utangulizi** .......... 3
**GESI ni nini?** .......... 4
**Nadharia yetu ya mabadiliko ya GESI ni ipi?** .......... 5
**Tunataka kuona mabadiliko gani?** .......... 8
Uwezo wa kufanya mambo .......... 8
Uwezeshaji .......... 8
Mabadiliko .......... 11
**Watu walio katika mazingira hatarishi ni watu gani?** .......... 12
Uchangamani .......... 13
**Tufanye nini ili kufanikisha lengo na madhumuni ya GESI?** .......... 14
Uchanganuzi na tathmini ya GESI .......... 16
Programu zinazolenga na kujumuisha GESI .......... 16
Mafunzo na kuendeleza uwezo wa wafanyakazi .......... 16
Zana na rasilimali za GESI .......... 17
Uandaaji wa bajeti na ufadhili .......... 17
Usanifu tathmini, ujifunzaji na kubadili .......... 17
**Utapata wapi taarifa zaidi?** .......... 19


# SHUKRANI


Mkabala na Nadharia ya Mabadiliko ya Usawa wa Kijinsia na Uhusishaji wa Kijamii (*kwa lugha ya kiingereza ni Gender Equality and Social Inclusion au kwa kifupi "GESI"*) wa shirika la World Vision uliandikwa na: Dr. Jacqueline Ogega, Mkurugenzi Mkuu wa GESI; Zayid Douglas, Mshauri Mtaalamu Mkuu wa GESI; Dr. Leticia Nkonya, Mshauri Mtaalamu Mkuu wa GESI; na Edward Winter, Mshauri Mtaalamu Mkuu wa GESI—pamoja na mchango kutoka kwa wawakilishi wa GESI katika idara mbalimbali za World Vision USA, na makao makuu ya World Vision.

Wachangiaji ni pamoja na Camilla Symes, Barbara Kalima-Phiri, Sarah Shteir, Brenda Wanjiku Kariuki, Sumera Jabeen, Ellie Wong, Kate Kobaidze, Tina Ojuka, Merydth Holte-McKenzie, Barbara Alupo, Shabira Nupur, Godfrey Senkaba, Jonathan Miller, Alisa Phillips, Lauren Zimmerman, Chloe Bass, Leo Hosh, Whitney Groves, Lisa Kingston, Mona Davies, Julie DeSoto, Lauren Van Enk, Alaina Bur na Chiedza Chinakwetu.

Ubunifu wa michoro: Stephanie Pierce-Conway, Pierce Conway Design

Shukrani za pekee kwa Dr. Leticia Nkonya na Aloisia Shemdoe kwa kufasili waraka huu.


*World Vision ni shirika la kidini la kusaidia watu lililojitoa kwa ajili ya kufanya kazi na watoto, familia, na jamii zao duniani kote ili kuwawezesha kufikia uwezo wao kikamilifu kwa kupambana na vyanzo vya umaskini na ukosefu wa haki.*



© 2023 World Vision, Inc.



Waraka huu unawasilisha **Mkabala na Nadharia ya Mabadiliko ya Usawa wa Kijinsia na Uhusishaji wa Kijamii ("GESI")** was shirika la World Vision. GESI ni muhimu katika kutimiza ahadi ya mikakati yetu mikubwa ya World Vision na malengo ya kuimarisha ustawi wa mtoto. World Vision kama shirika la kidini na kijamii linalomlenga mtoto, linahudumia watu wote bila kujali utaifa wao, rangi, dini, au jinsi.

Mkabala na Nadharia ya Mabadiliko ya GESI unatoa mwongozo wa jinsi ya kukamilisha hizo ahadi ili kufanikisha ustawi wa watoto, familia zao, na jamii iliyo katika maizingira hatarishi. Pia inachangia mafanikio ya mfumo mkuu wa vithibitisho vya mafanikio ya World Vision kwa kufanikisha malengo ya kuwa kiongozi wa mfano katika kufikia mabadiliko ya GESI yaliyothibitika.[1]

## AHADI YETU

Mkakati wetu unafanya kazi kwa lengo la kuwawezesha watoto, familia zao, na jamii zilizo katika mazingira hatarishi ili kubadili uhalisia wao na kujenga maisha ya baadaye yenye mafanikio.

1 Rejea World Vision's global impact framework and strategic initiative 2.2, which focus on capturing, utilizing and communicating evidence of impact..

# GESI
# NI NINI?

Shirika la World Vision linafasili GESI[2] **kama mchakato changamani wa mabadiliko** ambao:

**HUHIMIZA** usawa katika upataji na ufikiaji, ufanyaji maamuzi, ushiriki, na ustawi wa watu walioko katika mazingira hatarishi zaidi;

**HUBADILISHA** mifumo, desturi za kijamii, na mahusiano ili kuwawezesha watu walio katika mazingira hatarishi zaidi kushiriki na kufaidika kwa usawa katika afua za maendeleo;

**HUJENGA** uwezo wa kufanya mambo kwa mtu mmojammoja na kwa kikundi cha watu, uthabiti na matendo; na

**HUHIMIZA** uwezeshaji na ustawi wa watoto walio katika mazingira hatarishi, familia na jamii zao.

## Usawa wa **Kijinsia**

Hali inayowawezesha wanawake na wasichana, wanaume na wavulana, kufurahia kwa usawa haki za kibinadamu, mambo yanayothaminiwa na jamii, fursa, na rasilimali. Hii inajumuisha kuongeza uhuru na uwezo wa kutoa maoni, kuboresha mienendo ya kimamlaka na mahusiano, kubadilisha majukumu ya kijinsia na kuimarisha kiwango cha maisha kwa ujumla ili wanaume na wanawake waweze kutumia uwezo walionao kufanikisha malengo yao.[3]

## Uhusishaji wa **Kijamii**

Hushughulikia ukosefu wa usawa na/au uhusishaji kwa watu walio katika mazingira hatarishi kwa kutengeneza mazingira ya ushiriki katika jamii na kuboresha fursa, upataji na ufikiaji wa rasilimali, uwezo wa kutoa maoni na kuheshimu haki za binadamu. Unakusudia kuhimiza uwezeshaji na kuendeleza jamii na taasisi zenye amani.[4]

2 Refer to World Vision's GESI glossary of key definitions for additional concepts.
3 See UN Women; USAID Gender Equality and Female Empowerment Policy; and Naila Kabeer on empowerment.
4 Adapted from United Nations Sustainable Development Goals (SDGs), particularly SDG# 5, 8, 10, 11 and 16 which emphasize equality and inclusion.



# NADHARIA YETU YA MABADILIKO YA GESI NI IPI?

Lengo la Nadharia ya Mabadiliko ya GESI ya shirika la World Vision ni kujenga uelewa wa pamoja wa njia za mabadiliko zinazohitajika ili kufikia usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii, kukuza na kuongoza utaratibu mzuri wa ujumuishaji wa usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii katika na baina ya programu za sekta mbali mbali.

## Nadharia ya Mabadiliko ya GESI ya World Vision inasema kwamba:

### IKIWA

Wanawake na wasichana, wanaume na wavulana, watu wenye ulemavu na watu wengine walio katika mazingira hatarishi wana usawa katika **upataji na ufikiaji, ufanyaji maamuzi** na **ushiriki** katika ngazi za mtu binafsi, kaya, jamii na jumuiya;

**Mifumo** ina usawa, haki, na uhusishi katika ngazi za mtu binafsi, kaya, jamii na jumuiya; na kama

Watu walio katika mazingira hatarishi wana **ustawi** ulioimarishwa;

### BASI

Watu wanawezeshwa katika ufanyaji mambo, kutoa maoni na kufikia uwezo wao kamili;

Kaya zina usawa, haki, uwajibikaji wa pamoja na mahusiano yenye uwiano;

Jamii zinashiriki katika jitihada za pamoja, uhamasishaji, na uthabiti; na


Jumuiya zinaanzisha mifumo ya mabadiliko;

### KWA HIYO

**Watoto walio katika mazingira hatarishi, familia na jamii huyafurahia maisha katika ukamilifu wake.**

## Kuna VIKOA VITANO VYA MABADILIKO ya lazima ili kufikia mafanikio makubwa ya usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii.

### VIKOA VYA GESI VYA WORLD VISION




**UPATAJI NA UFIKIAJI**

Uwezo wa kupata na kufikia, kutumia, kudhibiti, na/au kumiliki mali, rasilimali, fursa, huduma, faida na miundombinu.

**UFANYAJI MAAMUZI**

Uwezo wa kufanya maamuzi bila kushurutishwa kwenye ngazi ya mtu binafsi, familia, jamii na jumuiya. Hii inajumuisha uwezo wa kudhibiti mali na uwezo wa kufanya maamuzi kwenye uongozi.

**USHIRIKI**

Uwezo wa kushiriki na kujihusisha kwenye masuala ya jumuiya na mifumo ya mamlaka ambayo yanashawishi na kuamua kuhusu maendeleo, shughuli za kimaisha na matokeo.

**MIFUMO**

Uwepo wa mifumo yenye usawa na jumuishi ambayo inahimiza uwiano, inayoshughulikia mahitaji mbalimbali ya makundi ya watu walio katika mazingira hatarishi na kutengeneza mazingira wezeshi kwa ajili ya uhusishwaji wao.

**USTAWI**

Hali ya kujisikia kuwa na thamani, uwezo, hadhi, kujiamini, heshima, usalama, afya, na ustawi wa kimwili, kihisia, kisaikolojia, na kiroho kwa ujumla. Hii ni pamoja na kuishi bila ukatili wa kijinsia na aina zote za unyanyapaa na ubaguzi.



**USTAWI** ni kigezo cha awali ili kuweza kunufaika na usawa na ujumuishaji katika upataji na ufikiaji, ufanyaji maamuzi, ushiriki, na mifumo. Bila **USTAWI**, watu walio katika mazingira hatarishi zaidi hawatahusishwa kwenye maboresho ya programu katika vikoa vingine; na *bila mabadiliko katika ufanyaji maamuzi, ushiriki, na mifumo, ustawi wao hautabadilika kwa baadae.*

Zaidi ya hayo, kama ambavyo ukandamizaji na ukosefu wa uhusishaji unavyoegemea kwenye mifumo na miundo ya jamii isiyo na usawa kama vile 'tabaka', 'jinsi' na 'ulemavu', vikoa vyote vinaathiriwa na miundo, desturi za jamii na mahusiano yaliyopo. Programu zote zinahitaji kubainisha na kushughulikia chanzo cha desturi na mahusiano ya kimamlaka yaliyopo ambayo yanaathiri vikoa vyote vitano vya GESI katika ngazi zote za mfumo wa ikolojia.

Nadharia ya Mabadiliko ya GESI ya shirika la World Vision imetokana na utendaji mzuri wa sasa na tafiti za usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii. Inaakisi mtazamo wa shirika la World Vision juu ya matokeo ya ustawi wa watu walio katika mazingira hatarishi zaidi kwa kuonyesha uhusiano uliopo kati ya vikoa vya GESI na ustawi.

# TUNATAKA KUONA MABADILIKO GANI?

Nadharia ya Mabadiliko ya GESI ya shirika la World Vision inajumuisha mifumo iliyochangamana na mikabala ya haki kuelekea kwenye ukuzaji wa usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii. Lengo la Mkabala wetu wa GESI ni kufikia uwezo wa kufanya mambo, uwezeshaji na mabadiliko ili kufanikisha vikoa vitano vya mabadiliko.

## UWEZO WA KUFANYA MAMBO

Mkabala wa GESI wa shirika la World Vision unawachukulia washiriki wa programu za maendeleo kama mawakala hai wa mabadiliko, na sio watu waliotengwa au wanufaika wa maendeleo wasio na mchango wowote. Mkabala wetu unaongeza uelewa wa kukuza uonyeshaji wa **uwezo wa kufanya mambo** ili watu walio katika mazingira hatarishi (na makundi) ambao awali walikuwa na uwezo/nguvu kidogo, kukuza uwezo wa kujitambua na kutoa mawazo yao, na kuwa na udhibiti juu ya maisha yao, rasilimali, imani, maadili, na mitazamo.[5] Uwezo wa kufanya mambo hupelekea kujiwezesha–**nguvu ya kufanya mambo** na **nguvu ya ndani**–kupitia ufahamu binafsi na mabadiliko ya mitazamo binafsi, jinsi mtu anavyojitazama na mahusiano ya kimamlaka. Washiriki wa programu hukuza ufahamu muhimu na hujiona wana uwezo, na wenye haki ya kuchagua, kufanya mambo, na kubadili maisha yao, kaya, jumuiya na jamii. Pamoja na mabadiliko binafsi, uwezo wa kufanya mambo pia hurahisisha uwezeshaji wa pamoja–**nguvu na**–kupitia mshikamano wa kijamii, harakati na jitihada za pamoja kwa ajili ya mabadiliko endelevu.[6]

## UWEZESHAJI

Mkabala wa GESI wa shirika la World Vision unafanikisha **uwezeshaji** kwa kuhoji miundo iliyojikita ya ukosefu wa usawa na uhusishaji, na kuongeza haki za binadamu, nguvu na uwezo wa watu walio katika mazingira hatarishi kufanya mambo. Ingawa uwezeshaji mara nyingi hutokea ndani ya mtu na hauwezi kufanywa na mtu yeyote au kwa ajili ya mtu mwingine, tamaduni, jamii na taasisi hutengeneza mazingira yanayorahisisha au kukandamiza uwezekano wa uwezeshaji.[7] Shirika la World Vision hutumia mikabala mbalimbali kuwezesha mabadiliko ya GESI katika programu.

5 Kabeer 1994; Sen, 1997; Batliwala, 1994; Rowlands 1997; Bill and Melinda Gates Foundation, 2018; CARE.
6 Rowlands discusses power when writing about the meaning of women's empowerment.
7 USAID Gender Equality and Female Empowerment Policy.

**Hii hujumuisha mikabala ambayo inatumika sana kama vile:**

| | |
|---|---|
| MODELI YA KIJAMII | Huchunguza jinsi miundo ya kijamii inavyo wanyang'anya watu nguvu na kuongeza ukosefu wa uhusishaji wa kijamii. Mkabala unasisitiza kuwa watu na makundi yaliyo katika mazingira hatarishi si tatizo; bali jamii inatakiwa kukabiliana na mahitaji, mitazamo na tofauti za watu, kama vile wasichana walio katika rika balehe na watu wenye ulemavu. |
| MAENDELEO CHANYA YA MTOTO NA KIJANA WA RIKA BALEHE | Huwawezesha watoto na vijana walio katika mazingira hatarishi pamoja na familia zao, jamii na/au jumuiya kufikia uwezo wao kamili. Afua zinajenga ujuzi, mali na ustadi; zinaongeza ushiriki wa mtoto, wasichana na wavulana walio katika rika balehe; zinachochea mahusiano bora; zinaimarisha mazingira wezeshi ya nje na kubadili mifumo.[8] |
| UHUSISHAJI WA WANAUME | Huwawezesha wanaume na wavulana kuwa washiriki na mawakala wa mabadiliko kupitia ukuzaji wa mitazamo mbadala iliyo chanya juu ya uanaume, ufanyaji maamuzi wa pamoja, usawa katika mgawanyo wa kazi kwenye utoaji huduma au kazi zisizo na malipo, mahusiano bora na ya kijinsia yanayozingatia usawa, yasiyo na ukatili, na kuondoa mila kandamizi kama vile ndoa za utotoni. |
| UWEZESHAJI WA WANAWAKE NA WASICHANA | Huwawezesha wanawake na wasichana kupata nguvu ya kufanya mambo kwa uhuru, kutumia haki zao, na kuishi maisha ya ukamilifu kama wanajamii kamili na wenye haki sawa. Inajumuisha afua za programu mahususi za GESI kwa ajili ya maendeleo ya uongozi na uwezeshaji wa kijamii na kitamaduni, kisiasa na kiuchumi kwa wanawake, wasichana walio katika rika balehe na mtoto wa kike. |
| UWEZESHAJI KIUCHUMI | Husaidia makundi yaliyokandamizwa kiuchumi kupata udhibiti wa kiuchumi, kifedha, mali na rasilimali. Uwezeshaji wa wanawake kiuchumi ni sehemu muhimu ya mkabala huu.[9] |

8 Youth Power 2019; World Vision Child Protection and Participation.
9 Bill and Melinda Gates Foundation Gender Equality Strategy focuses on WEE dimensions such as financial inclusion & services, knowledge, economic power & voice, and market opportunities.





## MABADILIKO

Mkabala na Nadharia ya Mabadiliko ya GESI unawezesha dhima ya shirika la World Vision na misingi yake kuhamasisha **mabadiliko** katika maisha ya watu kwa kuwafikia watoto walio katika mazingira hatarishi zaidi na kubadili hali zao.[10] Lengo ni kuhoji sababu za kina zinazosababisha mazingira hatarishi ambazo zinaendeleza ukosefu wa usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii, kama vile desturi za kijamii na kitamaduni, uhusiano usio na usawa na mifumo inayowanyang'anya baadhi ya watu nguvu. Mkabala wa mabadiliko unalenga katika kubadili **desturi za kijamii**, kuanzisha au kurejesha **uhusiano wa kijinsia na kijamii**, kuleta mabadiliko ya **kimuundo na kimfumo** (kiuchumi, kijamii, kisiasa au mengineyo), na kutengeneza **mazingira wezeshi** yanayofanikisha usawa na uhusishaji mkubwa.

Mabadiliko ya GESI yanahitaji **mabadiliko endelevu ndani ya mfumo wa ikolojia** ambao unazingatia uchangamani kati ya ngazi ya mtu binafsi, kaya, jumuiya na jamii. Ngazi hizi za kiikolojia zinaturuhusu kuelewa mlolongo wa sababu zinazo athiri usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii katika vikoa vitano vya GESI vya upataji na ufikiaji, ufanyaji maamuzi, ushiriki, mifumo, na ustawi.

10 World Vision's Transformational Development seeks to reach the most vulnerable children and their families, empower them and challenge the systems that cause poverty and vulnerability.

# WATU WALIO **KATIKA MAZINGIRA HATARISHI** NI WATU GANI?

Pamoja na kwamba mazingira hatarishi hutegemea muktadha, ushahidi unaonyesha kwamba ukosefu wa usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii unawaathiri zaidi watoto wa kike na wa kiume, wanawake, watu wenye ulemavu na watu wanaoishi katika umaskini. Sababu zingine za mazingira hatarishi au kutohusishwa ni pamoja na hadhi ya ukimbizi au uhamiaji, rangi, dini, umri, lugha na hali ya kiafya.

Shirika la World Vision linawatambua watoto walio katika mazingira hatarishi zaidi[11] kuwa ni wale wanaoishi na mambo mawili au zaidi kati ya haya yafuatayo:

- Wako katika mahusiano ya kunyanyaswa au unyonyaji;
- Wanaishi katika umaskini uliokithiri;
- Wanakabiliwa na ubaguzi mkubwa ambao unawazuia kupata na kufikia huduma na fursa; na
- Wako kwenye hatari kubwa ya kukabiliwa na athari hasi za maafa au majanga.




11 WVI Global Guidance on estimating the number of vulnerable children.

**World Vision inaboresha juhudi zake za kufanikisha maisha ya walio katika mazingira hatarishi kwa kuzingatia mahitaji ya watu.**

**TAMBUA |** Shirika la World Vision limejitolea kuwatambua kwa utaratibu maalumu watoto na watu wazima walio katika mazingira hatarishi zaidi, kutathmini mahitaji na hali zao mahususi, na kujumuisha michango yao katika miundo, utekelezaji, na ujifunzaji.

**HUSISHA |** Iwapo watu walio katika mazingira hatarishi zaidi, na mashirika yao, watahusishwa kikamilifu katika usanifu na utekelezaji wa programu, afua zitaendeleza usawa katika utoaji wa bidhaa na huduma, na washiriki wote watafaidika kwa usawa.

**SHIRIKIANA |** Ushirikiano unaoongozwa na wenyeji na unaozingatia mahitaji ya watu huhusisha watoto na watu wazima mbalimbali walio katika mazingira hatarishi zaidi. Hii ni pamoja na kushirikiana na mashirika yanaongozwa na watu walio katika mazingira hatarishi zaidi, mashirika yanayozingatia zaidi kukidhi mahitaji ya watu walio katika mazingira hatarsihi zaidi. Hii inamaanisha kuwathamini sio tu kwa sababu ya mahitaji yao, bali pia kwa sababu ya utaalamu, ujuzi, na uwezo wao wa kuongoza kwa ajili ya maendeleo endelevu.

**LINDA |** Kushirikiana na watu binafsi na vikundi vilivyo katika mazingira hatarishi ni pamoja na kulinda utu na ustawi wao wakati wote.

**JIFUNZE |** Kama shirika linalojifunza, World Vision inajitolea kutumia mbinu zenye ushahidi wa mafanikio, data ziliyogawanywa, mbinu mchanganyiko, tathmini za GESI, na majukwaa ya kujifunza ili kuendelea kuelimika na kuboresha maendeleo endelevu ya mabadiliko ya GESI na usaidizi wa watu wakati wa dharura.

## UCHANGAMANI

Watu hutofautiana na huwa wanajitambua kama sehemu ya vikundi tofauti tofauti, kwa hivyo kuna uchangamani kwenye ukosefu wa usawa au uhusishaji. Mkabala wa GESI unachunguza uchangamani au uhusiano wa mazingira hatarishi, ambao unaweza kusababishwa na ukosefu wa usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii vyote kwa wakati mmoja. Kwa mfano, wanawake wenye ulemavu wanaweza kukabiliwa na kutengwa maradufu kwa sababu ya tamaduni za kijinsia na unyanyapaa kwa watu wenye ulemavu. Hata hivyo, mwanamke mwenye ulemavu anaweza kuwa na viwango vya chini vya kutengwa ikiwa haishi katika umaskini na anapata na kufikia huduma na rasilimali kwa urahisi.

# TUFANYE NINI ILI KUFANIKISHA LENGO NA MADHUMUNI YA GESI?

Kuna mafanikio mengi makubwa ambayo yamefikiwa na shirika la World Vision katika kuhamasisha usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii, na kuweza kugusa maisha ya watu walio katika mazingira hatarishi zaidi kwa namna nzuri.

**Mkabala wa GESI unatokana na mafanikio yaliyotokana na kuweka kipaumbele maeneo 4 muhimu.**

**KUJUMUISHA** mikabala ya mabadiliko ya GESI kwenye kuongeza rasilimali, ikiwemo pendekezo la mradi, kujiweka tayari, na kuhusisha wafadhili.

**KUTUMIA** lenzi ya GESI kwenye utekelezaji wa programu kwa ajili ya kuhakiki ubora wa programu.

**KUIMARISHA** ukusanyaji wa ushahidi wa ufanisi wa GESI.

**KUHAMASISHA** muitikio wa GESI kwenye utendaji, sera, taratibu na mifumo ya uwajibikaji kwenye taasisi, na kutumia mwongozo wa kanuni za "kutoumiza wengine" na kanuni za kuwalinda.

Lengo ni kuwa na programu zenye mabadiliko ya GESI, kutathimini maendeleo kufuatana na jedwali la mwendelezo wa GESI wa shirika la World Vision.[12]

12 Adapted from the GESI Continuum in "DFID Girls' Education Challenge: Leave No Girl Behind Monitoring, Evaluation, and Learning Guidance" (July 2018); and the USAID IGWG Gender Integration Continuum (2017); WHO Gender Responsive Assessment Scale (2011).

<table>
<tr><th colspan="3">MWENDELEZO WA GESI WA SHIRIKA LA WORLD VISION</th><th>ALAMA</th></tr>
<tr><td rowspan="2">HAINA MUITIKIO WA GESI</td><td>Haina GESI</td><td>Haijali usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii.<br>• Haizingatii tofauti za kijinsia, ukosefu wa usawa wa kijinsia au uhusishaji wa kijamii.<br>• Kuna desturi za kibaguzi au kandamizi za kijamii, na mahusiano ya kimamlaka yasiyo na usawa, au uwezekano wa kukosekana usawa wa kijinsia au uhusishaji wa kijamii kwenye usanifu au utekelezaji wa shughuli za programu.<br>• Hakuna mjadala unaohusu jinsia au uhusishaji wa kijamii kwenye mambo mbali mbali ya shughuli za uendeshaji na jinsi hii inavyoweza kuathiri afua.</td><td>0</td></tr>
<tr><td>GESI ya Kinyonyaji</td><td>Inachochea kukosekana kwa usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii.<br>• Inatambua tatizo la ukosefu wa usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii, inatatafuta njia ya kuendelea kufanya shughuli zake, sambamba na hili tatizo, lakini haichukui hatua yoyote kutafuta ufumbuzi.<br>• Inachochea ubaguzi uliopo kwenye desturi mbaya za kijinsia na kijamii, tabia, mitazamo, majukumu na mahusiano.<br>• Inatumia fursa ya ukosefu wa usawa wa kijinsia, desturi za kijamii zenye ubaguzi, dhana potofu, miundo, na makundi katika jamii ili kufanikisha malengo yake.</td><td>1</td></tr>
<tr><td rowspan="2">INA MUITIKIO WA GESI</td><td>Inayojali GESI</td><td>Inatambua ukosefu wa usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii, inachukua hatua kupunguza hili tatizo lakini sio kuliondoa.<br>• Afua zinajumuisha mikakati maalumu ya kupunguza athari za ukosefu wa usawa na uhusishaji.<br>• Hujumuisha mahitaji halisi na uzoefu wa makundi yaliyo katika mazingira hatarishi lakini haitatui chanzo halisi cha tatizo la ukosefu wa usawa au uhusishaji.<br>• Kuna "fursa iliyopotea bure" ya kubadilisha desturi zinazochochea ukosefu wa usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii.</td><td>2<br>(+1)</td></tr>
<tr><td>Mabadiliko ya GESI</td><td>Inahamasisha usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii.<br>• Inapinga na kubadili desturi kandamizi za kijinsia na kijamii, dhana potofu, na mila za kibaguzi.<br>• Inabadili ukosefu wa usawa kwenye mahusiano ya kimamlaka, majukumu ya kijinsia, na mahusiano.<br>• Inalenga kujihusisha na kubadili ukosefu usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii.<br>• Inahamasisha usawa na uhusishaji kwenye upataji na ufikiaji, ufanyaji maamuzi, ushikiri, mifumo, na ustawi, kwa lengo la kufikia mabadiliko endelevu kuelekea kwenye usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii.</td><td>3<br>(+2)</td></tr>
<tr><td colspan="3">JUMLA YA ALAMA KWA PROGRAMU ZENYE MABADILIKO YA GESI</td><td>5</td></tr>
</table>

# BAADHI YA MIKAKATI YA KUFANIKISHA MABADILIKO YA GESI KWENYE PROGRAMU

## 1 UCHANGANUZI NA TATHMINI ZA GESI

- Fanya uchanganuzi wa GESI wakati wa mchakato wa kusanifu, kufanya utafiti wa awali na kama sehemu ya mwendelezo wa utekelezaji na tathmini ya progamu.[13]
- Tumia Mwendelezo wa GESI kutathmini maendeleo kwa kutumia vikoa 5 vya GESI, na kuelewa jinsi ya kubuni afua zenye ufanisi ambazo zinaelekea kwenye mabadiliko ya GESI.

## 2 PROGRAMU ZINAZOLENGA NA KUJUMUISHA GESI

- Buni afua za programu zinazolenga na kujumuisha GESI au shughuli zinazotokana na uchanganuzi wa GESI wa vikoa 5 vya GESI na ngazi za kijamii na kiikolojia.
- Tafuta na shirikiana na washirika maalumu waliobobea kwenye GESI, kama vile mashirika ya watu wenye ulemavu, mashirika ya haki za wanawake, mashirika ya ushiriki wa wanaume, wizara husika za serikali na watoa huduma maalumu.
- Tambua uhusiano wa mifumo iliyopo (kama vile ulinzi wa watoto, afya, na mifumo mingine) ambayo inatoa mkabala wa jinsi ya kutambua, kufuatilia na kusaidia programu za GESI kwenye makundi yaliyo katika mazingira hatarishi.

## 3 MAFUNZO NA KUKUZA UWEZO WA WAFANYAKAZI

- Toa mafunzo au ongeza uelewa wa GESI kwa wafanyakazi ili kuchanganua na kutafuta ufumbuzi wa desturi zitakazo athiri uwezo wao wa kusaidia makundi yaliyo katika mazingira hatarishi na kubainisha njia za kuhakikisha uhusishaji kwenye utekelezaji.
- Ajiri na hakikisha uwepo wa wafanyakazi na watu wanaojitolea wenye uwezo wa GESI na/au wanaowakilisha makundi yaliyo katika mazingira hatarishi.
- Unda uongozi wa GESI miongoni mwa wafanyakazi wa programu, ikiwemo kuanzisha wawakilishi wa GESI, jamii ya wataalamu wa GESI na mabingwa maalumu wa kisekta.
- Inapohitajika, tumia msaada wa kiutaalamu wa GESI kwenye usanifu, utekelezaji na kuripoti.
- Sambaza na tumia mara kwa mara sera na taratibu husika za taasisi kama vile; sera za ulinzi, utofauti wa watu, usalama na será zinazopinga unyanyasaji.

13 Refer to World Vision GESI DME toolkit for tools to conduct a GESI analysis.

## 4 ZANA NA RASILIMALI ZA GESI

- Tengeneza au tumia zana na rasilimali mpya ili kusaidia utekelezaji wa Mkabala na Nadharia yetu ya Mabadiliko ya GESI.
- Tumia zana na rasilimali zilizopo za shirika la World Vision zinazoonyesha mbinu zenye ubunifu na ufanisi kwa ajili ya mabadiliko ya GESI kwenye programu, kama vile; Sauti na Matendo ya Raia (Citizen Voice and Action), Njia za Matumaini (*Channels of Hope*), viunganishi vya miundo ya kijamii na kidini na uwezo wa kutumia imani iliojengwa kwa miaka mingi.
- Tumia zana kwa ajili ya uwajibikaji wa GESI, kama vile mwendelezo wa GESI, ili kutathmini maendeleo.
- Jumuisha GESI katika mipango ya kimkakati, michakato ya kuhuisha mikakati, mipango kazi ya mwaka na mapitio yanayoendelea kwa ajili ya kuweka vipaumbele, utekelezaji na ufuatiliaji wa maendeleo.

## 5 UANDAAJI WA BAJETI NA UFADHILI

- Hakikisha bajeti na na ufadhili wa GESI ni endelevu. Kwa mfano, kuanzisha mfuko wa GESI kutawezesha programu kulipia gharama za ziada ili kuimarisha uhusishaji wa makundi yaliyo katika mazingira hatarishi. Hii inaweza kuhusisha gharama kama utoaji wa huduma ya kulea watoto, kuwalipa wazazi au walezi ili wahudhurie hafla, ukalimani wa lugha ya alama, na utoaji wa vifaa vya kuwasaidia watu wenye ulemavu.

## 6 USANIFU, TATHMINI, UJIFUNZAJI NA KUKABILI

- Kusanya na tumia ushahidi na data bunifu za GESI—za kitaamuli na kitakwimu—ili kuongeza ushiriki, upataji na ufikiaji, ufanyaji maamuzi, ustawi na kubadili mifumo kwa ajili ya makundi yaliyo katika mazingira hatarishi.
- Unda na shirikisha wengine shughuli bora za GESI ili kusaidia miundo mipya, ujifunzaji shirikishi na kukabiliana na mambo.
- Pima ubora wa mikabala bunifu kwenye vyanzo mbalimbali vya ufahdili.
- Fanya tathmini za afua jumuishi za kila sekta na modeli za kipekee za shirika la World Vision, pamoja na Sauti na Matendo ya Raia (*Citizen Voice and Action*), Njia za Matumaini (*Channels of Hope*), mfuko wa uhusishaji, ufadhili na utumiaji wa miundo ya ulinzi wa mtoto na miundo mingine ya kuendeleza usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii.
- Onyesha uongozi wenye ushahidi katika GESI na imarisha chapa ya utaalamu ya shirika la World Vision.
- Imarisha ushirikishaji wa mashirika yanayofanana na lako, mashirika ya wafadhili, na taaluma. Wasilisha kuhusu GESI kwenye mikutano maalumu ya kisekta na ya GESI, pia andika machapisho yanayolenga GESI.



# Utapata wapi Habari zaidi?

Wasiliana na World Vision

**GESITeam@worldvision.org**

World Vision®